International Research Journal of Rongo University (IJORU) ISSN: 3005-7221
Transformative Research and Innovation for an Inclusive and Sustainable Future
Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

TAMADUNI NA SHERIA KANDAMIZI KATIKA TAMTHILIA YA JENEZA KUTOKA SAURABIA (2025)

[1]Francis Gathu*, [1]Sophie Okwena

*Corresponding Author: francisgathu618@gmail.com

https://orcid.org/0009-0005-0149-1686; https://orcid.org/0009-0007-9495-169X

[1]Chuo Kikuu Cha Taita Taveta, Sanduku la posta 635 – 80300 Voi, Kenya

Ikisiri

Utafiti huu unachunguza namna tamaduni na sheria kandamizi zinavyojitokeza katika Tamthilia ya Jeneza Kutoka Saurabia. Lengo kuu ni kufichua tamaduni na sheria kandamizi na athari zake kwa maisha ya wahusika. Licha ya kuwa tamaduni na sheria huwasilishwa kama mihimili ya utaratibu na maadili katika jamii, zinaweza kutumiwa kama nyenzo za ukandamizaji na unyanyasaji. Fasihi inachukuliwa kama chombo muhimu kinachoweza kufumbua macho ya jamii kwa kufichua ukweli uliojificha nyuma ya mila na taratibu zinazoonekana kuwa za kawaida. Ni kwa msingi huu ambapo utafiti huu unafanya uchambuzi wa kina kuhusu mwingiliano kati ya tamaduni na sheria kama mihimili miwili inayoweza kushirikiana kuendeleza ukandamizaji katika tamthilia ya Jeneza Kutoka Saurabia. Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Kijamii iliyoasisiwa na Marx na Engels (1848) ambayo inatoa mwanga angavu katika kuchambua masuala ya mamlaka, itikadi na upinzani wa wahusika dhidi ya mifumo dhalimu, na hivyo kuwezesha uelewa wa kina wa namna jamii inavyounda na kuhalalisha sheria zinazoweza kuathiri uhuru wa mtu binafsi. Utafiti huu umefanyika maktabani. Data imekusanywa kwa njia ya usomaji wa kina na uchambuzi wa suala la utamaduni na sheria kandamizi katika tamthilia teule. Sampuli lengwa ni tamthilia ya Jeneza kutoka Saurabia ambayo inashebeni masuala ibuka ya tamaduni na sheria kandamizi. Mbinu ya usampulishaji ambayo imetumika ni mbinu kusudio. Data iliyopatikana katika tamthilia teule imechanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti ambayo ni kuchunguza tamaduni na sheria kandamizi katika tamthilia ya Jeneza kutoka Saurabia. Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa imewasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji mifano. Matokeo yanaonyesha kuwa tamaduni na sheria kandamizi hutumika kama zana za kudhibiti na kunyima wahusika haki zao za msingi. Masuala ya tamaduni na sheria kandamizi yanadhihirika katika misingi ya kijinsia na kimadaraka, huku yakizua migogoro katika jamii. Hata hivyo, uwepo wa sauti za upinzani unaashiria mwamko na uwezekano wa mageuzi. Utafiti unapendekeza haja ya jamii kufanya tathmini upya ya mila na sheria zisizozingatia haki za binadamu. Isitoshe, makala hii inahimiza tafiti zaidi za kifasihi linganishi, ili kupanua upeo wa uelewa kuhusu mchango wa fasihi katika kupinga ukandamizaji na kuchochea mabadiliko chanya ya kijamii. Kwa jumla tamthilia ya Jeneza kutoka Saurabia inajadili masuala ibuka ambayo yamejumuishwa katika suala la Maendeleo Endelevu. Baadhi ya malengo ya maendeleo endelevu ni usawa wa kijinsia, afya, elimu bora na mengineyo ambayo mwandishi anaonyesha vile malengo haya yamepuuzwa kiasi cha kufanya mabinti kwenda kutafuta kazi ughaibuni ili kukidhi malengo hayo katika familia zao, jambo ambalo husababisha maafa na kurudishwa wakiwa wafu kwenye jeneza.

Maneno muhimu: *Miiko, sheria, tamaduni, ukandamizaji, Saurabia.*

Utangulizi

Tangu enzi za zama, fasihi, imekuwa ikitumika kama chombo cha kuelimisha, kuonya na kuashiria mwelekeo wa jamii. Katika mazingira ya sasa ambapo ulimwengu unakumbwa na changamoto nyingi za kijamii na kisiasa, umuhimu wa fasihi katika kutoa sauti kwa wasio na sauti unazidi kuonekana. Wamitila (2003) anasema kuwa tamthilia ikiwa ni utanzu unaoakisi matendo ya binadamu jukwaani, inatoa fursa ya pekee ya kuchambua mifumo ya mamlaka na jinsi inaathiri maisha ya kila siku ya wanajamii. Makala hii inajikita katika kuchambua tamthilia ya *Jeneza kutoka*

Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

Saurabia, kazi inayochochea fikira kuhusu uhusiano kati ya mwananchi, mila zake, na sheria zinazomtawala.

Utamaduni na sheria ni nguzo muhimu zinazoshirikiana kuimairisha na kudumisha amani, kutoa utambulisho kwa wanajamii na kujenga maadili. Lengo kuu la utamaduni ni kujenga utambulisho, maadili na mshikamano wa kijamii, na sheria kwa upande mwingine inalenga kulinda haki, kudumisha amani na kutoa adhabu rasmi kwa wale wanaokiuka.

Suala la tamaduni limekuwa likitazamwa kama uti wa mgongo wa utambulisho wa jamii yoyote ile. Hata hivyo, mwandishi wa tamthilia hii anaibua swali gumu: Je, inakuwaje pale utambulisho huo unapoanza kuwafunga na kuwakandamiza wale unaopaswa kulinda? Bhabha (1994) anaamini kuwa mamlaka ya sheria za kibeberu zinapojaribu kuongoza au kutengeneza jamii, zinashindwa kuwa kamili kwa sababu ya utata wa asili wa kibinadamu na upinzani wa kimya kimya au wa hila. Dhima ya sheria ni kulinda heshima ya nchi na kuadhibu kwa wanaoenda kinyume na taratibu zilizowekwa katika nchi hiyo. Aidha, sheria huimarisha haki na usawa kwa kulinda haki ya kila mtu na kusimamia raslimali za nchi na wala siyo kudhulumu na kunyayasa. Isitoshe, sheria yafaa kuzuia na kukomesha uhalifu kwa kuweka adhabu na kanuni zinazuia uvunjaji wa amani.

Mbaabu (1985) anasisitiza kuwa utamaduni ndio msingi wa fasihi na kwamba maisha ya jamii hayawezi kutenganishwa na jadi, desturi, vyakula na mfumo wa heshima. Mbaabu anaendelea kudai kuwa, lugha na fasihi hutirirka na kujengwa kutoka kwenye misingi imara ya utamaduni wa jamii husika. Vipengele muhimu vya utamaduni ni sanaa, lugha, desturi na mila. Utamaduni ni zana au mfumo unaomwezesha binadamu kukabili na kukidhi maslahi yake ya kibiolojia na kijamii katika mazingira yake (Malinowski 2014). Mtalaamu huyu anaendelea kudai kuwa, utamaduni humsaidia binadamu kukabili na kutatua matatizo ya maisha yake, na hivyo kuendeleza maisha ya jamii. Kwa hiyo, utamaduni unafaa kutekeleza lengo la kudhibiti maadili kwa kuonyesha miiko na miongozo ya namna wanajamii wanapasa kuishi na kuingiliana pamoja.

Kwa mujibu wa Tylor (2024), utamaduni ni ule mfumo tata unaojumuisha ujuzi, imani, sanaa, maadili, desturi na uwezo mwingine wowote au mazoea yanayopatikana kwa mtu kama mwanajamii. Utamaduni unachochoea stadi na mbinu za kuboresha maisha na mazingira ya kila siku na kjenga misingi bora ya maadili na mshikamano inayorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Naye Geetz (2017) anaona utamaduni kama mtandao wa maana au ishara ambazo binadamu mwenyewe amejifuma na kujenga mwongozo wa maisha yake. Utamaduni hujenga utambulisho kwa kuweka misingi ya desturi, mila na lugha zinazotambulisha jamii fulani kwa madhumuni ya kukuza msikamano kupitia kwa sanaa, sherehe na taratibu nyingine za jamii.

Kulingana na Essel (2018), sheria hudumisha miiko na nidhamu. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kwamba miiko na desturi za kitamaduni zina dhima ya kulinda jamii dhidi ya matendo maovu na kuimarisha misingi ya maadili. Lakini sheria hizi, badala ya kuwa mhimili wa haki kulingana na Essel, zimekuwa nyenzo za unyanyasaji zinazotumiwa na tabaka tawala kudumisha hali iliyopo. Hali hii inasababisha migogoro ya kisaikolojia na ya kijamii ambayo inahitaji uchunguzi wa kina. Naye Durkheim (2013) aliona sheria kama kielelezo cha mshikamano wa jamii. Alisema kuwa aina ya sheria katika jamii hubadilika kulingana na mfumo wa maisha. Aligawa sheria katika *sheria za adhabu* (kwa jamii za jadi zenye mshikamano wa pamoja) na *sheria za fidia* au urejesho (kwa jamii za kisasa zenye mgawayo wa kazi).

Weber (1954) anatoa maoni kwamba, sheria ni mfumo uliopangwa ambao unatawaliwa na mamlaka na nguvu ya kiserikali. Anaendelea kusema kuwa katika jamii za kisasa sheria imekuwa ya kiufundi na yenye kufuta taratibu za kiakili na kisheria badala ya kutegemea mila au desturi za zamani pekee. Sheria ni nyenzo inayotumiwa na jamii kutatua migogoro, kusawazisha maslahi yanayokinzana, na kuongoza maendeleo ya kijamii kwa njia ya haki (Pound, 2012). Utamaduni ni jinsi binadamu anavyokabili maisha, kujumuisha maadili, lugha na shughuli za kila siku zinazitambulisha shughuli fulani.

Umuhimu wa utafiti huu unajidhihirisha katika mazingira ya sasa ambapo usawa wa kijinsia na haki za msingi za binadamu ni vipaumbele katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kama yalivyoanishwa na Umoja wa Mataifa (2015). Kwa kuanika uozo wa mifumo kandamizi katika kazi ya fasihi, utafiti huu unachangia katika mwamko wa kijamii unaohitajika kwa ajili ya mabadiliko.

Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

Msingi wa Nadharia

Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Kijamii iliyoasisiwa na Marx na Engels (1848). Kiini cha nadharia hii ni kuchunguza uhusiano uliopo kati ya kazi za fasihi na jamii. Mtazamo wa nadharia hii ni kuwa fasihi ni zao la mazingira ya kijamii ya mwandishi. Kama anavyofafanua Eagleton (2002), nadharia hii inasisitiza kuwa kazi ya fasihi haitoki kwenye ombwe, bali ni zao la mazingira maalum ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Nadharia ya Uhakiki wa Kijamii inachunguza kazi za kifasihi kama zao la jamii. Inasisitiza kuwa fasihi haitoki hewani; inahusiana moja kwa moja na siasa, uchumi, historia, na utamaduni. Inawalazimu wahakiki kuangazia jinsi maudhui yanavyoakisi matabaka, nguvu, na mapambano ya wanajamii. Mihimili mikuu ya nadharia hii inajumuisha mambo yafuatayo:

Kwanza, kazi ya fasihi inapaswa kuakisi hali halisi ya maisha na matatizo ya wanajamii kama vile umaskini, ukosefu wa ajira, na ufisadi kwa vile fasihi ni kioo. Pili, huchunguza migogoro kati ya wanyonyaji (wenye mamlaka/mali) na wanyonge (wanaokandamizwa) ndani ya jamii. Tatu, wahusika katika kazi ya fasihi husawiriwa kama watu halisi au makundi ya watu katika jamii. Matendo yao, migogoro yao, na maamuzi yao yanawakilisha jamii husika. Nne, nadharia inahimiza uchunguzi wa msimamo wa mwandishi na itikadi inayotetea ili kuleta mabadiliko chanya katika.

Aidha, Wafula na Njogu (2007) wanabainisha kuwa uhakiki wa kijamii husaidia kuanika migogoro ya kitabaka na jinsi wanyonge wanavyoweza kutumia sauti zao kupinga mifumo dhalimu. Kupitia nadharia hii, inabainika jinsi mwandishi anavyotumia wahusika kama wawakilishi wa makundi mbalimbali katika jamii, kudhihirisha kundi la wale wanaofaidika , na lile linaoumizwa . Nadharia ya Uhakiki wa Kijamii unatusaidia kufichua itikadi zilizofichika nyuma ya maneno ya wahusika na matukio yanayotokea katika tamthilia, na hivyo kutoa mwanga kuhusu mustakabali wa jamii hiyo.

Uhakiki wa Maandishi

Wasomi kadhaa wamejadili dhima ya fasihi ya Kiswahili katika kuangazia ukandamizaji na ukombozi wa kijamii. Kwa mfano, Wamitila (2003) anabainisha kuwa tamthilia ni utanzu hai unaofaa zaidi kuanika mifumo ya mamlaka na jinsi inavyoathiri maisha ya kila siku ya raia wa kawaida. Aidha, Mbatiah (2018) anasisitiza kuwa uhakiki wa kijamii katika fasihi unapaswa kujikita katika kufafanua migogoro ya wahusika kwani wao ndio nguzo kuu ya kubeba maudhui ya kijamii. Ingawa wasomi kama vile Wamitila (2003) na Mbatiah (2018) wametoa mchango mkubwa katika kuonyesha jinsi tamthilia inavyoakisi mifumo ya mamlaka na migogoro ya wahusika kijamii, na huku wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wakielekeza nguvu zao katika kuchambua ukandamizaji wa kisiasa au ubaguzi wa kijinsia kama masuala yanayojitegemea, tafiti zao zimeacha upungufu wa kimtazamo. Tatizo la utafiti huu linatokana na ukweli kwamba, ingawa wasomi wengi wamechambua ukandamizaji wa kisiasa katika fasihi ya Kiswahili, bado kuna uhitaji mkubwa wa kuangazia jinsi tamaduni na sheria zinavyoingiliana kuunda mfumo mmoja dhalimu. Mara nyingi, tamaduni hutazamwa kama suala la kijamii na sheria kama shughuli ya kiserikali, lakini katika *Jeneza kutoka Saurabia*, viwili hivi vinafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Pengo hili la maarifa ndilo ambalo utafiti huu unalenga kuliziba, kwa kuonyesha kuwa huwezi kupambana na sheria kandamizi bila kwanza kuelewa mizizi ya kiutamaduni inayozirutubisha.

Wasomi hawa waliofanya tafiti zilizotangulia mara nyingi wamemiliki mwelekeo wa kutazama tamaduni kama jambo la kijamii linalojitenga na sheria, ambayo nayo hutazamwa tu kama chombo cha kiserikali. Pengo hili la maarifa ndilo linalozibwa kikamilifu na utafiti huu wa sasa. Tofauti na mitazamo ya wasomi waliotangulia, utafiti huu unaonyesha mwingiliano wa karibu na wa kimkakati kati ya tamaduni na sheria kama mihimili miwili inayoshirikiana kuendeleza ukandamizaji wa kitabaka na kirangi katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*.

Mbinu za Utafiti

Muundo wa utafiti ni ramani inayomwongoza mtafiti katika kupata majibu ya maswali ya utafiti (Ritchie na Lewis 2003). Utafiti huu ni wa aina ya kimaelezo. Muundo wa kimaelezo ulitumiwa kwa kuwa umetoa maelezo kuhusu tamaduni kandamizi katika tamthilia teule ya *Jeneza kutoka Saurabia (2025)*

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Sehemu hii imekuwa msaada kwa watafiti kwa vile imesaidia kupata data ambayo ni ya uhakika na ya kuaminika. Katika maktaba, watafiti walisoma vyanzo mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti pamoja na kutafuta ufahamu zaidi wa nadharia zilizotumika kuchanganua data. Katika upekuzi huu, makala, tasnifu, majarida, viu machapisho muhimu yanayohusu tafiti mbalimbali

Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

zilizowahi kufanywa kuhusu tungo za Kithaka Mberia yalipitiwa. Waaidha, utafiti wa maktabani ulinuia kupata data kutokana na usomaji mpana wa tamthilia teule ya Kithaka ya *Jeneza kutoka Saurabia* (2025)

Katika usampulishaji, mbinu kusudio ilitumika. Mbinu kusudio ilitumika kuteua tamthilia teule ya Kithaka wa Mberia, *Jeneza kutoka Saurabia* ambayo inasheheni tamaduni na sheria kandamizi. Mbinu kusudio ni faafu pale ambapo sehemu fulani ya sampuli inaaminika kuwa ina data faafu inayoafiki malengo ya utafiti (Kombo na Trump 2006). Kadhalika, mbinu kusudio huwa haizingatii ukubwa wa sampuli bali cha muhimu ni ikiwa sampuli yenyewe inamwezesha mtafiti kupata data toshelevu ambayo inashughulikia suala la utafiti kikamilifu (Lune, 2010).

Data ilipatikana kwa kusoma kwa kina tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia*. Data hiyo ilijenga msingi wa kufafanulia tamaduni na sheria kandamizi. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo huku akitoa mifano ya kushadidia hoja zilizotolewa.

Utamaduni kandamizi

Utamaduni ni neno pana linalorejelea amali, imani, desturi, maarifa na tabia ambazo watu wa jamii husika hujifunza na kurithishana kizazi hadi kizazi, (Tylor, 2024). Kwa hiyo, utamaduni kandamizi ni mfumo wa mila, desturi au mitazamo ya kijamii inayowadhulumu, kuwanyonya au kuwanyima haki na uhuru wanyonge uhuru wao. Mifano ya utaduni kandamizi ni kama vile ukatili wa kijinsia, ndoa za utotoni, ubaguzi wa rangi, kuzuia wanawake kupata elimu au kumiliki mali nk. Kwa ufupi utamaduni unajumuisha mambo yafuatayo: Lugha, mavazi, chakula, imani na dini, sanaa na burudani na miiko.

Katika tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia*, Mberia anadhihirisha ukandamizaji wa kiutamaduni kupitia ubaguzi wa rangi, ukatili wa kijinsia na mavazi.

Nambi na Sharifa ni wahusika wanaotumiwa kufichua au kuweka wazi tamaduni ambazo ni kandamizi katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*. Imani kuwa watu wenye rangi nyeusi ni watu ovyo, ni mojawapo ya tamaduni kandamizi ambapo Nambi anaonekana kuwa mtu ovyo na Sharifa. Sharifa analalamikia Anwar kwa sababu ya kumletea mfanyakazi ambaye ana ngozi nyeusi. Haya yanadhihirika katika maongezi kati ya Sharifa na Anwar:

Sharifa: Tulikubaliana nini?

Anwar: Nitafute mfanyakazi

Sharifa: Basi, ikawaje?

Anwar: Nikatafuta mfanyakazi

Sharifa: Ukaona ni sawa kuniletea ngozi nyeusi (uk. 22)

Dhana ya kuwaona watu wenye ngozi nyeusi kama watu ovyo ni imani potovu ambayo imepaliliwa tangu zamani tangu karne ya kumi na saba. Ni imani ambayo imepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Pia imani hiyo ni mfano wa tamaduni kandamizi ambayo watu wenye asili ya Kiarabu wamerithi kutoka kwa wazee wao waliotangul. Vygotsky (2012) anashadidia maoni haya kwa kudokeza kwamba, mambo ya kijamii na kiutamaduni yana ushawishi mkubwa katika ukuaji wa akili, tabia, na mfumo wa kujifunza wa binadamu kupitia mwingiliano wa jamii. Sharifa aliona Waafrika kama watu walioachwa au kubaki nyuma katika maendeleo. Imani hii ilikuzwa na kuzidi kukita mizizi kwa kuwa hata katika karne ya ishirini na moja bado Waafrika wanaonekana kama watu mabaradhuli na vizazi vya watawala wa Kiarabu. Sharifa anamdhihaki Nambi kwa kusema:

Sharifa: Unaonekana kama akili yako ni bora kuliko ngozi yako. (uk. 26).

Kutokana na muktadha wa usemi hapo juu, Sharifa amegubikwa na kasumba kwamba mtu mweusi hana akili na hii ndiyo sababu analinganisha akili ya Nambi na ngozi yake. Huu ni utamaduni potovu ambao amekua na kulelewa nao.

Aidha, Sharifa anamkaripia Nambi pindi anajaribu kukaribia palipo na sinia na kukagua chakula:

Sharifa: Zuzu! Gulagula! Zumbukuku! Bwege! Dutu! Uliniambia kabla ya kutoka kuondoka

msituni Afrika ulionyeshwa jinsi ya kupika. Unadhubutu kutuletea matabwatabwa!

Yachukue urudi nayo jikoni ukapike chakula baradhuli kabisa! (uk. 27).

Dhana na imani kuwa Afrika ni msitu wa mabaradhuli, zumbukuku na mabwege, ni sehemu ya utamaduni ambao kwa kweli unatumiwa kukandamiza wenye asili ya Kiafrika kama Nambi. Haya madai ni ya kuonyesha Waafrika kama watu ambao hawajaendelea na kuwa hawana maarifa yoyote na kwamba wameachwa nyuma kimaendeleo. Kutokana na muktadha wa mifano hapo juu, inadhihirika kuwa kulingana na utamaduni wa

Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

Saurabia, watoto hukuzwa na kulelewa na wazazi wao na kasumba kwamba watu weusi hawana akili na hakuna lolote nzuri wanaloweza kulitekeleza kwa 'akili yao nyeusi'. Sharifa amelewa na wazazi wake akifundishwa hivyo na hii ndiyo sababu anapomwona Nambi anaanza kumdharau kwa sababu ya weusi wake kiasi kwamba anamtusi na kumwita majina inavyodhihirika hapo juu.

Kithaka pia anaonyesha utamaduni kandamizi kupitia kipengele cha mavazi. Nambi analazimishwa kuvua nguo alizokuwa amevaa sababu kwamba sio za heshima kulingana na utamaduni wa Saurabia. Nambi na Halima wanapofika katika Ufalme wa Saurabia, Zakiya ambaye ni mhudumu anakagua Nambi kwa macho makali na bila kusema lolote na anaondoka:

Zakiya: (*kwa Halima*) Wewe ni nani?

Halima: Halima

Zakiya: (*kwa Nambi*) Na wewe?

Nambi: Nambi.

Zakiya: Hebu nyanyuka. (*Nambi ananyanyuka. Zakiya anamkagua kimo kama kwamba*

anampima urefu kwa macho. Anatoka)

Nambi: Sijui kwa nini amenikagua kwa macho vile.

Halima: Sikuelewa. Labda tutajua hivi punde.

Nambi: Sijui nguo zangu zina nini.

Halima: Naziona safi.

Zakiya: (*baada ya kurudi akiwa na vazi mkononi. Kwa Nambi*). Shika! (*Akiashiria sehemu*

ambayo imetengwa na pazia). Ingia humo uvue hilo vazi lako. Linakejeli imani na

maadili. Vaa hili. (*Nambi anainuka na kuingia katika sehemu ambayo ameonyeshwa…*)

Halima: Ni kawaida ya Wakristo kuvaa kama alivyovaa.

Zakiya: Hamkujua mnakuja katika nchi ya amani?...(kur 15-16).

Kulingana na usemi hapo juu, Ufalme wa Saurabia unashikilia utamaduni wa Uislamu wa wanawake kuvaa buibui au abaya ili kusitiri mwili wote. Kuvaa mavazi ya Kiislamu siyo utamaduni kandamizi bali shida inatokea pale Nambi anaonekana kama kwamba hafai machoni mwa Zakiya na kusahau kwamba hata Nambi ana utamaduni wake wa Kikristo. Zakiya hakumkalisha Nambi chini ili amweleze vile anafaa kuvaa akifika Saurabia, bali akimkagua kwa macho ya dharau kisha akatoka bila kusema lolote na kumletea vazi ambalo alimlazimisha kuvaa bila maelezo yoyote.

Sheria kandamizi

Sheria ni mfumo wa kanuni ambazo kwa kawaida hutekelezwa kupitia taratibu fulani za nchi (Pound, 2012). Hivyo, sheria kandamizi ni kanuni au sheria zinazodhulumu, umiza, kubana na kunyima wananchi haki zao za kimsingi. Sheria kandamizi zina sifa zifuatazo; zinalinda watawala na kudhulumu wananchi, inazuia uhuru wa kutoa maoni, kukusanyika, kusema, hutoa masharti magumu na adhabu kali.

Katika tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia*, Mberia anadhihirisha sheria kandamizi kupitia utoaji wa masharti magumu na adhabu kali na kunyimwa uhuru kusema na kutoa maoni.

Nambi anapofanya kazi kwa miezi minne bila kulipwa mshahara, ananyimwa haki ya kusema na kutoa maoni yake kuhusu kulipwa mshahara. Nambi anapodai kulipwa mshahara wake, Sharifa anamwambia kwamba analamika. Yanavyodhihirika hapa chini:

Nambi: Memsahib, nitapata mshahara lini?

Sharifa: Mshahara! Mshahara! Mshahara! Unauliza kuhusu mshahara. Umefanya kazi

kwa muda gani?

Nambi: Miezi minne, Memsahib

Sharifa: Miezi minne pekee pekee! Miezi minne pekee na unathubutu kuniuliza

mshahara?…

Sharifa: Nakuuliza unalalamikia mshahara au hulalamikii mshahara?

Nambi: Nauliza tu

Sharifa: Bado hunijibu. Ni malalamishi au si malalamishi kuhusu mshahara? (uk35)

Kutokana na muktadha wa usemi kati ya Nambi na mwajiri wake hapo juu, inabainika kwamba Nambi hana haki ya kusema au kutoa maoni yake. Hii ni sheria ambayo kina Sharifa wanatumia kunyamazisha wafanyikazi wao. Yaani kudai ulipwe mshahara wako imechukuliwa kama malalamishi.

Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

Aidha, Kithaka anaonyesha sheria zinazonyima wananchi haki zao za kimsingi. Nambi ananyimwa mshahara wake ambao amefanyia kazi kwa muda wa miezi minne. Hata baada ya Nambi kumwambia Sharifa kwamba aliacha mtoto wake na mamake ambaye anaishi katika lindi la umasikini, Sharifa anamwambia kwamba hawakujulishwa kwamba wanapagazwa jukumu la kulea wasioweza kujilea:

Nambi: Mtoto wangu nyumbani hana mtu mwingine wa kumtegemea. Nilimwacha na

mamangu ambaye kiuchumi hajiwezi. Mama anaishi katika shimo la ufukara.

Hawezi kumsaidia mtoto wangu…

Sharifa: Wakala aliyelipwa pesa na wakala wa mume wangu hakutueleza kwamba

alipanga kutupagaza jukumu la kulea wasioweza kujilea...hadithi zako ni ngeni

kwetu. Mambo yaliyo mbali,, mbali katika bara jingine yanatuhusu nini?

(kur 35-36)

Kutokana na muktadha wa mazungumzo hapo juu, ni dhahiri kwamba Nambi amenyimwa haki zake za kimsingi za kushughulikia na kukimu mahitaji ya mtoto wake ambayo ndiyo sababu kuu alimfanya kuenda ughaibuni kutafuta riziki.

Isitoshe Nambi ananyimwa haki za kibnafsi akiwa ughaibuni ambao ni ukandamizaji wa kisheria:

Nambi: ..Naomba tu mnilipe mshahara wa miezi mitano niliyowafanyia kazi.

Sharifa: Uamuzi wa wakati wa kulipa ni la waajiri wako. Mfanyikazi hana uwezo wa

kujiamulia wakati wa kulipwa….

Nambi: Kama sitalipwa leo, naomba nipate pesa japo kidogo … ninunue bidhaa za

dharura

Sharifa: Bidhaa za dharura gani?

Nambi: Nahitaji bidhaa za kibnafsi

Sharifa: Nakuuliza swali kwa lugha wazi nawe unatia jawabu katika ukungu?

Nambi: Wewe kama mwanamke mwenza unanielewa ninaposema, “Bidhaa za

kibnafsi”

Sharifa: Ni nani unamwita mwanamke mwenza? Unaniona mimi kuwa sawa na wewe? …

Nambi: Namaanisha mwenzangu kimaumbile; siyo kijamii…

Sharifa: (*kwa kelele*) Nyamaza…

Sharifa: Kwa nini hukuleta “bidhaa za kibnafsi” za kutosha? (kur 36-37)

Kupitia na maongezi ambayo yanadhihirika hapo juu, Nambi ananyimwa hata mahitaji ya kimsingi ya kila mwanamke. Mahitaji haya ya kibnafsi ni muhimu kwa kila mwana wa kike ambapo anaomba alipwe mshahara wake japo kidogo aweze kujinunulia “mahitaji ya kibinafsi” Sharifa anajifanya kwamba hana habari cha kile Nambi anahitaji.

Kadhalika, Nambi ananyimwa haki za kimsingi kama afya au siha ya kimwili anapougua. Nambi hashughulikiwi wala hapewi muda wa kutulia anapougua. Kwa sababu yeye ni mfanyikazi, afanye kazi akiumwa kama ni kufa afe:

Sharifa: Hii ni picha gani unanionyesha? Nilidhani unafanya kazi kumbe umetulia

jikoni kama mjusi ukutani.

Nambi: Naumwa sana.

Sharifa: Unaumwa na Ndwele au uzembe?

Nambi: Ndwele bila shaka.

Sharifa: Wapi haswa?

Nambi: Tumbo.

Sharifa: Tumbo tena? Juzi ulisema unaumwa tumbo...jana ukaniambia

una uchungu...Nina uwezo wa kutabiri..

Nambi: [*kwa hadhira*] Kuna maisha yanayoeleweka na yasiyoeleweka; hali ya

kustahimilika na isiyostahimilika; mateso yanayovumilika na yasiyovumilika.

Chakula kinachoweza kuitwa chakula sipati; usingizi wa kutosha kuondoa

machovu silali; heshima anayostahili binadamu, kwangu ni ndoto ya mbali kama

nyota angani. Nikijaribu kuuliza swali najipata kwenye chaka la kinamasi; chaka

lenye pogoo kavu zinazoporomoka na kunigonga kichwani; chaka lenye ukungu

unaoziba njia mtu asijue pa kukanyaga. (uk 31)

Mazumgumzo hapo juu yanaonyesha vile afya ya Nambi siyo muhimu kwa waajiri wake na huu ni ukiukaji wa haki za kimsingi ambao ni ukandamizaji kisheria.

Waaidha, Nambi ananyimwa hata chakula, suala ambalo ni hitaji la kimsingi na huu ni ukandamizaji wa sheria:

Nasrat:...Nieleze shida zako bila kufumbafumba lugha.

Nambi: Hivi ninapozungumza nawe, sijala kwa siku mbili

Nasrat: Kwa nini?

Nambi: Kwa sababu ya kunyimwa chakula na waajiri wangu

Nasrat: Kwa nini wanakunyima chakula?

Nambi: Naona ni kama ni jambo linalowafurahisha…(kur 61-62)

Mazungumzo kati ya Nambi na Nasrat yanatokea baada ya Nambi kutoroka nyumbani kwa waajiri wake hadi kituo cha polisi kutafuta usaidizi. Kulingana na muktadha wa mzungumzo inabainika kwamba Nambi ananyimwa hata chakula. Ukandamizai wa sheria unajumuisha kunyima mtu haki zake za kimsingi zikiwemo chakula, malazi nk.

Haki za Nambi zinakiukwa wakati Sharifa anasongoa pua ya Nambi na kumtukana baada ya kukwepa kofi lake. Huu ni ukandamizaji wa kisheria kwa sababu sheria kandamizi ni sheria zinazodhulumu na kuumiza:

Sharifa: kwa nini ukaja huku badala ya kutafuta kazi mahali pengine?

Nambi: Kama maisha ni haya, afadhali niuondokee ustaarabu

nirudi ambako, kutokana na kutojua, unakuita msituni.

Sharifa: Ukinitusi nitahakikisha huo ulimi umegura kinywa chako.

Nambi: Sijakutusi na wala sina haja ya kukutusi. Ninachotaka ni mshahara wangu

niende zangu.

Sharifa: Endelea kutoa sauti kama nyani mtini.

Nambi: Usiniite nyani

Sharifa: (*akimlenga kofi ambalo Nambi anakwepa*) Wewe mtumwa mweusi kama

makaa ya mawe! Unathubutu kuniambia nisilopaswa kufanya? (*Ghafla anashika*

pua ya Nambi na kujaribu kuisongoa…) (kur 38-39)

Anwar, mume wake Sharifa anataka kumdhulumu Nambi kimapenzi ambao ni ukandanizaji wa kisheria kwa vile sheria kandamizi ni sheria zinazodhulumu na kuumiza mtu. Dhuluma inaweza kuwa ya kisaikolojia, kimapenzi n.k. Anwar anauliza Nambi maswali ya kibnafi kama iwapo ana mume nyumbani. Swali ambalo Nambi analiona kwamba ni la kibnafsi na nia yake sio nzuri kwa sababu halina uhusiano na kazi anayofanya:

Anwar:...Nyambani una mume? (*Nambi anashangazwa na swali: ananyamaza)*

Nimekuuliza kama una mume?

Nambi: Bw. Anwar, sipendi kuongea maisha yangu ya kibnasfi

Anwar: Unafanya kazi kwangu. Hakuna ubaya wa kunijibu…

Nambi:...Naomba nisikujibu swali kwa sababu halina uhusiano na kazi

yangu hapa nyumbani mwako.

Anwar: Unajua vipi halina uhusiano?

Nambi: Kwangu kuwa na mume au kutokuwa na mume hakuwezi kuathiri

ninavyofanya kazi.

Anwar: Ndivyo unavyofikiria lakini…

Anwar: Kazi za nyumbani zina sura nyingi.

Nambi: Sura zipi Bwana Anwar?

Anwar: ….za kuchosha na za …..kusisimua (*kimya*) Nijibu…

Anwar: Weka kifyonza vumbi pale uje uketi hapa..

Nambi:...(*Anwar anasongeza kiti chake tena karibu na kile cha Nambi. Nambi*

anasongeza ili kuongeza umbali baina yao)

Anwar: Ukiruhusu tuwe pamoja, maisha yako yatabadilika….miili yetu ikiwa marafiki,

nitakulipa mshahara wako wote mara moja… (kur 54-57)

Kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Anwar na Nambi, inabainika kwamba Anwar ana nia ya kumdhulumu Nambi kimapenzi na hii ndiyo sababu ambayo imemfanya hajamlipa mshahara wake kwa vile anamwambia kwamba "miili yetu ikiwa marafiki, nitakulipa mshahara wako wote mara moja"

Haki ya Halima ya kutoa maoni na kusikizwa inakiukwa wakati anajaribu kudokeza ukweli kuhusu kifo cha Nambi kwamba Nambi mwenyewe alimwarifu kwamba alikuwa anatishiwa na kifo. Halima alidokeza kwamba kifo cha Nambi huenda kilisababishwa na mama mwenye nyumba ambaye ni Sharifa. Maoni ya Halima yanapuuzwa na chifu wa eneo hilo ambaye anawakilisha serikali:

Mchungaji: Kuna mgeni ambaye anafanya kazi na Nambi katika Ufalme wa Saurabia.

Tunamshukuru sana kwa kuomba ruhusa kutoka kwa mwajiri wake na

kujilipia tikiti ili kuhudhuria mazishi ya Nambi. Tumpe nafasi aseme mawili

matatu.

Halima: Naitwa Halima. Tulikutana na Nambi tukiingia Ufalme wa Saurabia tukaanza

kuongea. Ingawa tulikuwa hatukutani ana kwa ana tulikuwa tukiongea kwa

simu. Sina mengi ya kusema ila haya matatu: Kwanza, Nambi alikuwa mtu wa

kujiheshimu; pili, alifanya kazi kwa bidii nyingi. La tatu ambalo ni muhimu

kuliko yote, Nambi aliniambia anatishiwa na kifo. Sijui kama ni kweli alijitoa

roho au uhai wake ulitolewa na mama mwenye nyumba alikokuwa akifanya

kazi. Baada ya kifo cha Nambi, nilipigia ubalozi simu na nikawaeleza

wafanyikazi kuhusu changamoto zilizokuwa zikimkumba Nambi ikiwa ni

pamoja na kupigwa na kutishiwa kifo. Pia nimezitoa habari hizo kwa shirika

la kutetea haki.

Nyatio: Bwana Chifu anayasikia hayo?

Chifu: Nayasikia.

Nyatio: Kwa hiyo?

Chifu: Kama kuna habari tofauti na tulizotumiwa na serikali, serikali itajua na

itatufahamisha.

Mchungaji: Maombi yatakuwa mafupi sana…. (Nyatio anamunyamunya maneno).

Unasemaje Nyatio? (Nyatio anaanguka….). ...Tuendelee na mazishi

Nyatio: (sauti ya kukokota) Hatuendelei.

Mchungaji: Itakuaje?

Nyatio: Ukweli kwanza….

Mchungaji: Sikuelewi.

Nyatio: Tupelekee Serikali maiti.

Chifu: (*kwa kushtuka*) Kwa nia gani?

Nyatio: Ya kupata ukweli…

Chifu: Hilo haliwezekani. Laweza hata kusababisha nifutwe kazi. Kila wanapokufa,

serikali yetu na wazazi wa marehemu, huambiwa aliyefarika alijitoa uhai

mwenyewe...Kila serikali inapoambiwa hivyo, kama bwege, kama juha, kama

gulagula haiulizi maswali. Haishughuliki na kusaka ukweli kuhusu vifo. Hilo ni

tofauti na nchi nyingine zilizo na wafanyikazi ughaibuni.

Chifu: Wewe! Umekuja kumzika mwenzako au kuwachochea watu dhidi ya serikali?

Halima: Kuutafuta ukweli si uchochezi….

Halima: ...kuna vijana wengi wanaofia

Saurabia na nchi za Masharika ya kati kila mwaka… Serikali inapaswa

kuhakikisha usalama wa wananchi wakiwa ndani na nje ya nchi...(kur 83-87).

Kulingana na muktadha wa mazungumzo, yaelekea kwamba Chifu mwenyewe anataka kuficha ukweli kuhusu kifo cha Nambi ambao ni ukandamizaji wa

Received 27/06/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 13/10/2026

kisheria. Halima anapoelezea ukweli wa mambo jinsi yalivyo, Chifu anapuuza na kumwambia kwamba anachochea watu. Chifu ambaye anafaa kulinda na kutunza sheria, ndiye anayezivunja kwa kudai kwamba jambo hilo litafanya afutwe kazi yake. Kwake Chifu kazi yake ni muhimu kuliko maisha ya vijana wengi ambao wameuwawa katika Ufalme wa Saurabia.

Kithaka pia anaonyesha ukandamazaji wa sheria wakati Nambi anapoenda kituo cha polisi kutafuta usaidizi ambao hakupata. Nambi anaamua kukimbia kutoka kwa waajiri wake kutokana na dhuluma hizi. Licha ya maafisa wa polisi Abuwalid na Nasrat kuwa na nia ya kumsaidia Nambi, wanapata kuwa "mikono" yao au uwezo wa kumsaidia Nambi umefungwa na 'sheria za kafala' ambazo zinampa mamlaka mwajiri kufanya atakavyo na mfanyakazi wake:

Abuwalid: (*kwa Nasrat*) Wakubwa wameendelea na mkutano zaidi ya muda

niliokadiria

Nasrat: (*akimwashiria Nambi)* Amekuja kutafuta usaidizi

Abuwalid: (*kwa Nambi*) Ungependa usaidizi gani?

Nambi: Nina hamu ya kwenda nyumbani

Abuwalid: Sikuelewi.

Nambi: Ningependa kurudi nchini mwangu.

Abuwalid: Nchi yako ni gani?

Nambi: Nyake

Abuwalid: Ulikuja huku kufanya kazi?

Nambi: Ndiyo, kufanya kazi

Abuwalid: Gani?

Nambi: Ya nyumbani

Abuwalid: Muda mliokubaliana na mwajiri wako umekwisha?

Nambi: Bado.

Abuwalid: Basi kwa nini unataka kurudi kwenu kabla ya kumaliza….?

Nambi: Maisha siyo kama nilivyo...

Abuwalid: Kuna nini?

Nambi: Silipwi mshahara, sipewi chakula na ninadhulumiwa kimwili na kiakili

Abuwalid: ...Ulipotoka kwenu kuja huku kufanya kazi ulielezwa sheria zinazosimamia

kazi huku? ….

Nambi: Baadhi

Abuwalid: Ulielezwa kuhusu Sheria ya Kafala?

Nambi: Sikumbuki. (kur 63-64)

Kulingana na muktadha wa mazungumzo hapo juu, ni kwamba licha ya kuwa sheria ndiyo tumaini la mwisho kwa Nambi katika kujikomboa, sheria iyo hiyo anayoitegemea ndiyo inayodumaza hatua zake za kukimbia udhalimu aliokuwa akitendewa na Sharifa na Abuwalid. Sheria kandamizi inayojitokeza katika tamthilia hii ni mfumo rasmi wa kisheria wa *Kafala*, unaotumika katika nchi za Kiarabu kudhibiti hadhi ya sheria ya wafanyakazi wa kigeni. Nambi anapoamua kukimbia kutoka kwa waajiri wake kutokana na dhuluma anazopitia, maafisa wa polisi Abuwalid na Nasrat, licha ya kuwa na nia njema ya kumsaidia, wanagundua kuwa uwezo wao wa kumsaidia umefungwa na sheria za Kafala zinazompa mwajiri mamlaka kamili juu ya mfanyakazi wake ikiwa ni pamoja na kudhibiti pasipoti yake hazingewaruhusu. Mawazo haya yanatibitishwa na Marx (2021) ambaye aliona sheria kama chombo kinachotumiwa na kundi lenye nguvu za kiuchumi (tabaka tawala) kulinda maslahi yao na kuwakandamiza wananchi wanyonge katika mfumo wa kibepari. Marx anaendelea kusema kwamba sheria, serikali na vyombo vya dola ni sehemu ya muundo wa juu unaodhitiwa na wale wanaomiliki njia kuu za uzalishaji. Kwamba, njia za kibepari zimeundwa kulinda mali binafsi na unyonyaji wa nguvu za kazi za wanyonge. Mtalaamu huyu aliamini kuwa usawa mbele ya sheria ni wa uongo kwa sababu sheria inatoa faida kwa wenye pesa na kuwakandamiza maskini wanaokosa raslmali za kujitetea.

Ijapokuwa mikataba ya kimataifa inayosimamiwa na Umoja wa Mataifa (2015) inatambua haki za wafanyakazi wahamiaji kama haki za binadamu zisizoweza kunyimwa sheria za ndani za baadhi ya nchi, kama mfumo wa *Kafala* unavyoonyeshwa katika tamthilia hii, mara nyingi hupewa nguvu zaidi kuliko viwango hivyo vya kimataifa. Pengo hili kati ya sheria za kimataifa zenye nia njema na utekelezaji halisi wa sheria za ndani ndilo linaloendeleza mateso ya wahusika kama Nambi.

Hitimisho

Utafiti huu umedhihirisha kuwa tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* ni kioo makini kinachoakisi uozo wa mifumo ya kijamii na kisheria inayokandamiza utu wa binadamu. Kupitia uchambuzi wa wahusika kama Nambi na Sharifa, imebainika kuwa tamaduni zilizopitwa na wakati na sheria dhalimu kama mfumo wa Kafala zinafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu ili kudumisha sheria za utabaka, ubaguzi wa rangi na unyanyasaji wa kijinsia. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa fasihi ina uwezo wa kipekee wa kuibua sauti za wanyonge na kuweka wazi itikadi zilizojificha nyuma ya pazia la mila na desturi, hivyo kutoa mwito wa mabadiliko ya dharura katika mitazamo ya kijamii na mifumo ya utawala ili kuhakikisha haki na usawa kwa wote.

Mapendekezo

Utafiti unasisitiza haja ya jamii kufanya tathmini ya kina na endelevu ya amali na imani zake ili kuondoa zile zinazokiuka haki za kimsingi za binadamu chini ya mwavuli wa utambulisho. Serikali na mashirika ya kimataifa yanapaswa kushirikiana katika kufanya mageuzi ya kisheria yatakayowalinda wafanyakazi, wahamiaji na makundi yaliyo pembezoni dhidi ya sheria kandamizi zinazowafanya kuwa mali ya waajiri wao. Aidha, wasomi wa fasihi wanahimizwa kufanya tafiti linganishi zaidi kati ya tamthilia za Afrika Mashariki na zile za Mashariki ya Kati ili kupanua uelewa wa mwingiliano wa kitamaduni na jinsi unavyoathiri maendeleo ya kijamii. Hii itasaidia katika kuunda mazingira yanayozingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa lengo la kumi la kuhimiza usawa.

Marejeleo

Bhabha, H. (1994). *The Location of Culture*. London: Routledge.

Durkheim, E. (2013). *Durkheim and the Law*. Palgrave Macmillan

Eagleton, T. (2002). *Marxism and Lliterary Ccriticism*. Routledge

Essel, E. (2018). "The Role of Taboos in African Governance System". In Econimic and Social journal

Geertz, C. (2017). *The Interpretation of Cultures*. USA: Basic Books

Kombo, D. & Trump, D. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Nairobi: Parlines Publication Africa.

Lune, H. (2010). *Perspectives in social research methods and analysis*. Thousand Oaks: Sage Publication Inc.

Malinowski (2014). *A Scientific Theory of Culture and other Essays*. Routledge.

Marx, K. (2021). *The Research Handbook on Law and Marxism*. Edward Elgar Publishing.

Mbaabu, I. (1985). *Swahili Culture and Society*. Nairobi: Kenya Publishing & Book Marketing

Mbatiah, M. (2018). *Fasihi na jamii*. Nairobi: Longhorn.

Mberia, K. (2025). *Jeneza Kutoka Saurabia*. Nairobi: Marimba publishers Limited.

Pound, R. (2012). *Jurisprudence*. USA: LawBooks Exchange Ltd.

Ritchie, J. & Lewis, J. (2003). *Qualitative research practice: A guide for social sciences students and researchers*. London: Sage Publications.

Tylor, E.B. (2024). *Primitive Culture Research into the Development of Mythiology Philosophy and Religion, Art and Custom*. London: Dover Publication.

Vygotsky, L. (1986). *Thought and Language*. MIT Press.

United General Assembly (2015) *Transforming our world*: The 2030 Agenda For Sustainable Development. (Resolution A/RES/70/1. United Nations

Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2003). *Msingi cha uchambuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa

Publishers.

Weber, M. (1954). *Max Weber on Law in Economy and Society.* USA. Harvard University Press.